# Jarida la KILIMO

Toleo la Nane

ISSN: 1821- 8113

Oktoba - Disemba, 2011



*Mhe. Ramadhan A. Shaaban Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili akikabidhi vyeti kwa wahitimu wa mafunzo ya cheti cha kilimo katika mahafali ya 10 yaliyofanyika tarehe 31/12/2011 Chuo cha Kilimo Kizimbani, Wilaya ya Magharibi Unguja.*

## Yaliyomo

Maoni ya Mhariri/ Picha ya Jalada.....Uk.2
Matayarisho ya Upandaji Miche ya Mikarafuu.....Uk.3
Umuhimu wa Chanjo kwa Mifugo.....Uk.4
Popo wa Pemba.....Uk.5
Programu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Kifedha Vijijini.....Uk.6 - 7
Matukio katika Picha.....Uk.8 - 9
Mahafali ya 10 ya Chuo cha Kilimo Kizimbani.....Uk.10
Mchango wa TASAF katika Usarifu wa Mazao.....Uk.11
Usarifu wa Mazao ya Kilimo.....Uk.12-13
Umwagiliaji Maji ndani ya Greenhouse.....Uk.14
Mafanikio katika Bonde la Kianga Mwembe Msala.....Uk. 15-16

## Bodi ya Wahariri

Washauri
Affan O. Maalim
Juma Ali Juma
Dk. Bakar S. Asseid

Mhariri Mkuu
Dk. Juma M. Akil

Msanifu na Mhariri Mtendaji
Hashim H. Chande

Wahariri Wasaidizi

Makame M. Abdulrahman

Nassor S. Mkarafuu

Nassor S. Mohammed

Mpiga chapa
Fatma A. Juma

Mpiga picha
Khamis A. Bakari



ANUWANI
Wizara ya Kilimo, Maliasili - Zanzibar
S.L.P. 159
Simu: +255 24 2230986
Fax: +255 24 2234650
E-mail: kilimo@zanlink.com
Tovuti: kilimoznz.or.tz


# MAONI YA MHARIRI

Ndugu Wakulima, kuja kwa programu ya masoko, uongezaji thamani na huduma za kifedha vijijini [MIVARF] kutaongeza fursa nyingi za utoaji wa ajira vijijini.

Makamo wa pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi aliyasema hayo huko Bwawani tarehe 29-11-2011 wakati alipokua akizindua programu hii yenye lengo la kusukuma mbele maendeleo ya wakulima, wafugaji na wavuvi hasa walioko vijijini ambao hukabiliwa na hali ngumu ya maisha.

Ndugu Wakulima, hii ni moja kati ya hatua za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano na washirika wa maendeleo kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili katika jitihada zake za kuleta mapinduzi ya kilimo ambapo utekelezaji wa programu hii ndio utakaoongeza uzalishaji pamoja na matumizi ya teknolojia za kisasa na kuongeza kipato kitakachosaidia kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Ndugu Wakulima, Sekta ya kilimo husaidia upatikanaji wa ajira kwa asilimia 70 kwa wananchi wake na kuchangia asilimia 50 ya chakula ambacho tunakizalisha. Sekta hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa nchi inajitosheleza kwa chakula na kuweza kumkomboa mwananchi kuondokana na umasikini. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikichukua juhudi kwa mashirikiano na watendaji wa Sekta ya Kilimo kuandaa miradi mbali mbali na kuwafikishia wananchi walioko vijijini.

Ndugu Wakulima, programu ya MIVARF imekusudia kuinua kipato cha wakulima, wafugaji na wavuvi wa vijijini pamoja na kuwasaidia kuondokana na uzalishaji duni, ukosefu wa masoko na usafirishaji wa bidhaa zikiwa ni miongoni mwa changamoto zinazowakabili walengwa hao, hivyo ujaji wa MIVARF utaleta mafanikio kama yalivyopatikana kupitia programu zilizotangulia za PADEP na ASSP/ASDP-L na wananchi walivyoweza kunufaika.

Ndugu Wakulima, wakati wa uzinduzi wa mradi huu akitoa nasaha zake Mhe. Balozi Seif amefahamisha kuwa programu hii ya MIVARF ni muendelezo wa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Programu mbili zilizotangulia kati ya hizo ni pamoja na Pogramu ya Uendeshaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo na Huduma za Kifedha Vijijini ambapo Programu hizo mbili zilitekelezwa katika baadhi ya Mikoa ya Tanzania Bara kwa kipindi cha 2002-2010 na walengwa wa programu hizo waliweza kunufaika kwa ujenzi wa masoko pamoja na ukarabati wa maghala na barabara pamoja na kumuongezea mkulima kipato chake.

Ndugu Wakulima, Programu ya MIVARF ina uwezo mkubwa wa kuleta mafanikio na kumkomboa mkulima na mfugaji kutokana na hali duni ya maisha. Aidha, Balozi Seif alisema ujaji wa Programu hiyo uende sambamba na kuwawezesha wananchi kukabiliana na ushindani wa soko katika ulimwengu huu wa utandawazi na kuzijengea uwezo asasi za wakulima pia kupanua wigo kwa wazalishaji na wasiokua wazalishaji pamoja na kuwapa fursa ya kuamua hatma ya maisha yao.

Ndugu Wakulima, kuwepo kwa programu ya MIVARF ni moja ya hatua muhimu ya kuweza kujiletea maendeleo katika nchi yetu kama malengo yataweza kufikiwa na hapana budi jitihada za makusudi zichukuliwe ili kufikia malengo yaliyowekwa katika utekelezaji wa Programu hiyo. Aidha, ni matarajio ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili iwapo walengwa wote watatimiza wajibu wao na kusimamia ipasavyo malengo ya programu hii uzalishaji utaongezeka, kipato, uhakika wa chakula vijijini na hatimae kupunguza umasikini.

# PICHA YA JALADA

Katika picha anaonekana Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban akikabidhi vyeti kwa wahitimu wa mafunzo ya kilimo katika mahafali ya 10 yaliyofanyika tarehe 31/12/2011 Chuo cha Kilimo Kizimbani, Wilaya ya Magharibi Unguja. Akiwa pamoja na viongozi wengine wa Wizara ya Kilimo na Wizara nyengine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

# MATAYARISHO YA UPANDAJI WA MICHE YA MIKARAFU KWA MSIMU WA MASIKA 2012

Na Rashid Khamis

Zao la karafuu ni muhimu kwa uchumi wa Zanzibar na linachangia katika pato la wakulima na Taifa kwa ujumla. Katika msimu wa karafuu za mwaka uliopita 2011 kiasi cha Shilingi bilioni 63 zililipwa kwa wakulima baada ya kuuza tani 4,214 za karafuu kwa Shirika la Taifa la Biashara la Zanzibar (ZSTC), ambapo fedha hizo zilizopatikana zinawasaidia wakulima na wananchi wote.

Historia ya Zanzibar inaonyesha kwamba takriban karne mbili zimepita tangu Zanzibar ilipoanza kuotesha mikarafuu. Tokea wakati huo kushamiri kwa zao hilo kunatokana na juhudi zinazochukuliwa za kutayarisha miche, kupanda na kuhudumia mashamba hayo.

Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka tayari inaendelea na uzalishaji wa miche ya mikarafuu ambapo kwa mwaka 2011/12 imepanga kuzalisha kiasi cha miche laki tano (500,000) na inatarajiwa kutolewa bure kwa wakulima katika msimu huu wa masika. Hivyo wakulima mnaombwa kufanya matayarisho ya mashamba yenu mapema.

Utayarishaji na upandaji wa miche ya mikarafuu unaanza kwa kuchagua eneo lenye ardhi nzuri kwa ustawi wa mikarafuu. Kwa Unguja ardhi nzuri ni zenye udongo wa kinongo ambazo zinapatikana Wilaya za Kaskazini A na B pamoja na Wilaya za Magharibi na Kati. Sehemu kubwa ya ardhi ya Pemba ina udongo wa aina ya Bopwe na Utasi, ambazo ni ardhi nzuri kwa uoteshaji mikarafuu.



Baadhi ya miche ya mikarafuu iliyozalishwa katika vitalu vya serikali ikisubiri kugaiwa kwa wananchi ili kupandwa katika mashamba yao msimu wa masika 2012

Wakulima wanashauriwa wasipande mikarafuu kwenye mabonde yanayotuama maji, maeneo ya uwandani na yenye kina kidogo cha udongo kwani husababisha kufa kwa mikarafuu. Vilevile, jua kali wakati wa kiangazi kwa baadhi ya maeneo yanayopata mvua chache husababisha kukauka kwa unyevu ardhini na kusababisha kufa kwa mikarafuu kwa vile miti hii inahitaji mvua nyingi zipatazo wastani wa milimita 2,000 hadi 3,000 kwa mwaka.

Mikarafuu inatakiwa ipandwe kwenye mistari iliyonyooka kwa masafa ya mita 8 hadi 10 wastani wa hatua za mtu mzima 9 hadi 11, ni muhimu kupanda kwa masafa yanayopendekezwa ili mikarafuu iweze kustawi vizuri na kuweza kutoa mavuno mengi. Mavuno yatapungua ikiwa mikarafuu itapandwa karibu au mbali sana kutoka mche mmoja hadi mwengine. Upandaji unashauriwa ufanyike pale ambapo mvua za masika zimeshamiri.

Mashimo ya kupanda yatayarishwe kabla ya kuchukua miche ya mikarafuu kutoka kwenye vitalu. Mche wa mkarafuu unahitaji shimo la sentimita 45 kwa sehemu zote yaani upana na urefu. Wakati wa kuchimba shimo tenganisha udongo wa tabaka ya juu na ya chini, kwa kawaida udongo wa tabaka la juu una virutubisho vingi zaidi kuliko ule wa chini, hivyo ni vyema kutanguliza tabaka la juu wakati wa kupanda. Mashimo yaliyotayarishwa vizuri kwa ajili ya upandaji wa mikarafuu yanasaidia miche kuishi na kukua vizuri.

# UMUHIMU WA CHANJO KWA MIFUGO

Na Nassor S. Mohammed

Mifugo ni rasilimali ambayo huwapa faida kubwa wafugaji na wananchi wa Zanzibar. Ili mifugo itoe mazao yenye tija inahitaji kupatiwa huduma bora za malisho, maji, kinga na tiba za maradhi. Maradhi ni moja kati ya matatatizo yanayozorotesha sekta ya ufugaji na kupunguza uzalishaji. Katika kukabiliana na changamoto hiyo hatua za kuyadhibiti maradhi zinachukuliwa duniani kote ili kuimarisha ufugaji na kupata tija.

**Chanjo**
Chanjo ni mchanganyiko maalum wenye vijidudu ambavyo vimepunguzwa nguvu ili visilete madhara kwa wanyama au watu waliochanjwa. Hii ni njia mojawapo inayotumika katika kudhibiti maradhi duniani

Asili ya chanjo ilitokana na ugunduzi wa mwanasayansi wa Uingereza Bw. Edward Jenner katika karne ya 18 ambapo aligundua kwamba wahudumu wa ng'ombe hawakupata ugonjwa aina ya ndui (small pox) kutokana na kuwa na vijidudu vya ugonjwa wa ndui za ng'ombe (cow pox) hali ya kuwa maeneo mengine wasiokuwa wahudumu wa ng'ombe waligundulika kuwa na ugonjwa huo.

Chanjo husababisha mwili wa mnyama au binadamu kuandaa askari (vikinga mwili ni antibody) ambao hukaa mwilini kwa muda maalum na huukinga mwili kukabiliana na vijidudu vya maradhi. Aidha, chanjo ikipungua nguvu inahitajika wanyama wachanjwe tena kwa muda maalum uliopendekezwa kutokana na aina ya chanjo au mnyama.

**Aina za chanjo**
Miongoni mwa chanjo maarufu zinazotumika kwa mifugo ni; Hitcher B1, LaSota, S19/ Rev- 1 strain, Blanthrax, Rabisin, Tetanus Toxoid, Newcastle Disease vaccine EDS – 76 + ND + IBD, Fowl pox, Clon CL/76 strain, Canine distemper, Marek's disease vaccine, Foot and Mouth Disease, Gumboro, Mahepe/Mdondo/Kideri, Ndui, Pepopunda, Kimeta, Chambavu, Ugonjwa wa kutupa mimba kwa ng'ombe, Ugonjwa wa mapafu wa ng'ombe na mbuzi, Ugonjwa wa bonde la ufa, Ugonjwa wa ngozi (Lumpy skin, Streptothricosis, Warts, Mange) Ugonjwa wa miguu na midomo,

**Maradhi yanayochanjwa na muda unaopendekezwa.**
Chanjo ya Gumboro kwa kuku




Miongoni mwa chanjo maarufu zinazotumika kuchanja/kuzuia maradhi ya mifugo kama Foot and Mouth Disease, Gumboro, Mahepe/Mdondo/Kideri, Pepopunda, Kimeta na Chambavu.

wachanga mara moja katika uhai wake;
Chanjo ya Mahepe/Mdondo/Kideri kwa kuku mara mbili katika uhai wake;
Chanjo ya Ndui kwa kuku na ng'ombe mara moja;
Chanjo ya ugonjwa wa kutupa mimba kwa ng'ombe mara moja kwa mwaka;
Chanjo ya ugonjwa wa Kimeta kwa ng'ombe kila mwaka;
Chanjo ya ugonjwa wa Chambavu kwa ng'ombe kila mwaka;
Chanjo ya ugonjwa wa pepopunda (Tetenasi ) kwa ng'ombe kila mwaka;
Chanjo ya ugonjwa wa ngozi kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo kila mwaka;
Chanjo ya ugonjwa wa miguu na midomo kwa ng'ombe kila mwaka;
Chanjo ya ugonjwa wa homa ya mapafu kwa ng'ombe na mbuzi kila mwaka;
Chanjo ya Kichaa cha mbwa kwa mbwa kila mwaka;
Chanjo ya ugonjwa wa matumbo hasa kwa mbwa wadogo pia unaweza kuchanja kwa wakubwa kila mwaka;
Chanjo ya Ugonjwa wa sotoka kwa ng'ombe kila mwaka;
Chanjo ya ugonjwa wa bonde la Ufa kwa ng'ombe;
Chanjo ya ugonjwa wa Farasi kwa farasi kila mwaka.

**Wanyama wanaochanjwa**
Wanyama hao ni pamoja na ng'ombe, mbuzi kondoo, nyati, ngamia, mbwa, paka, farasi na jamii ya ndege wakiwemo kuku wa aina zote wa mayai nyama na wa kienyeji.

**Faida za Chanjo**
- Chanjo hudhibiti magonjwa yanayosababishwa na vimelea vya aina ya virusi, bektiria, rikesia na protozoa;
- Chanjo huongeza uwezo wa mnyama kujikinga na maradhi;
- Chanjo hulinda afya ya mifugo baada ya lishe bora na;
- Chanjo hudhibiti magonjwa yasiyoweza kutibika.

**Njia na sehemu za kuchanja**
- Kupitia mdomoni kwa magonjwa ya mahepe/mdondo/kideri, Gumboro kwa kuku;
- Kwenye bawa kwa ugonjwa wa ndui kwa kuku;
- Chini ya ngozi kwa magonjwa kama ya ngozi.

**Mambo ya kuzingatia katika uchanjaji**
Chanjo zihifadhiwe kwenye hali ya ubaridi na zisiwekwe kwenye joto au mwanga wa jua, wanyama wanaochanjwa ni lazima wawe na afya nzuri na hawajaambukizwa magonjwa yaliyokusudiwa kuchanjwa. Inashauriwa chanjo zifanywe na wataalamu wa mifugo au wafugaji waliopewa mafunzo ya kuchanja.

Chanjo zinaweza kuleta madhara ikiwa zitatumiwa wakati muda wake wa matumizi umekwisha (expired). Aidha, chanjo zenye vijidudu vilivyohai zinaweza kuambukiza maradhi kwa wanyama waliochanjwa.

'KINGA NI BORA KULIKO TIBA' .

# POPO WA PEMBA

Na Hashim H. Chande



Popo wa Pemba wakiwa katika maeneo yao ya msitu wa Hifadhi Ole Kidike

Popo ni viumbe wa ajabu, ambao watu wanaendelea kubishana kwamba ni ndege au mnyama, lakini pamoja na hayo viumbe hawa wanachangia katika utunzaji wa mazingira na inakadiriwa kwamba kiasi cha asilimia 40 ya miti ya matunda inayoota misituni katika kisiwa cha Pemba husambazwa na popo hao.

Jumuiya inayohifadhi mazingira kisiwani Pemba "KIDIKE" iliyopo Ole, Wilaya ya Wete, Pemba iliyoanzishwa mwaka 1992 ni jumuiya ambayo inaendeleza kazi ya kuwahifadhi viumbe hao ambao ni adimu zaidi duniani na ni miongoni mwa viumbe ambao wako hatarini kutoweka. Kufuatia utafiti uliofanyika mwaka huo ambao uligundua kuwa kiasi cha popo wa Pemba 101 tu ndio waliohamia katika msitu huo mdogo wa Ole Kidike. Hivyo, hatua za kulifanya eneo hilo kuwa tengefu zilichukuliwa sambamba na kuweka ulinzi na kuwaelimisha wanajamii umuhimu wa kuwepo na kuwatunza popo wa Pemba.

Katika kuunga mkono juhudi za wananchi hao za uhifadhi wa mazingira ikiwemo upandaji wa miti na uhifadhi wa popo wa Pemba , Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (MACEMP) uliwasaidia kutengeneza kidungu maalum kwa ajili ya wageni wanaokwenda kuangalia popo hao, ushajiishaji wa uhifadhi wa popo wa Pemba kwa kupitia vyombo vya habari kama vile redio, magazeti na televisheni, kuwapatia wananchi elimu ya mazingira pamoja na uwekaji wa mabango maalum ya utoaji wa taarifa zinazotambulisha kuwepo kwa sehemu ya uhifadhi, utambulisho wa miti adimu na sehemu za historia za uhifadhi huo.

Kupatiwa ufadhili huo umeweza pia kusaidia harakati za kijamii pembezoni mwa hifadhi hiyo kwa kuwawezesha wanajamii kujikusanya pamoja na kuanzisha miradi midogo midogo ya kazi za mikono kama vile kutengeneza matenga kwa kutumia muwaa, vyungu na mikoba bidhaa ambazo huwauzia watalii wanaofika katika hifadhi hiyo na kujiongezea kipato. Aidha, mapato yanayopatikana kwa kuingia wageni katika msitu huo kuangalia popo wa Pemba na uhifadhi wa mazingira pia yanatumika kusaidia maendeleo ya jamii.

Kuwepo kwa popo hao katika eneo hilo kunachangia kwa kiasi kikubwa uingiaji wa wageni kutoka nje ya nchi kwa ajili ya utalii pamoja na kazi za utafiti. Mbali na kazi za utafiti na utalii inaaminika kwamba asilimia kubwa ya popo wa Pemba wanasaidia harakati za usambazaji wa mbegu za miti hasa ya matunda kama vile miembe na mibungo hudondoshwa na popo hao.

Popo wa Pemba wanakawaida ya kula matunda na kutembea na kokwa za matunda hayo wanapozidondosha ndio miti hiyo huota. Kwa kawaida Popo hao wana uwezo wa kusafiri umbali wa kilomita 15 hadi 20 wakati wa usiku kutafuta chakula, hivyo inawezekana kabisa kwa popo wa KIDIKE akafuata chakula katika msitu wa Ngezi na akaangusha mbegu za miti ya matunda katika eneo la Limbani, Wete wakati wa kurudi.

Miti ambayo popo wa Pemba wanapendelea kulala ni migulele, misufi, mikungu, milangilangi pamoja na miembe ambayo kawaida huwa mirefu sana. Hadi kufikia mwaka 2010 inakadiriwa msitu wa Kidike ulikua na popo wasiopungua 7,700 hali inayotokana na mafanikio makubwa ya Jumuiya ya Uhifadhi wa Mazingira ya KIDIKE kwa kuwatunza na kuwaendeleza kwani kuongezeka kwa popo hao kunaongeza kasi ya uotaji wa miti katika sehemu mbalimbali.

Licha ya ongezeko kubwa la popo hao katika msitu wa Kidike pia imegundulika kwamba kuna baadhi ya maeneo kama vile Wete Bandarini, Msitu wa Ngezi, Kichunjuu Mkoani na Micheweni popo hawa wanapatikana hivyo, ipo haja ya kuzishajiisha jamii zinazoishi katika maeneo hayo kuanzisha jumuiya za uhifadhi wa popo wa Pemba ili kuwalinda popo hao, kwa faida ya jamii husika na serikali kwa lengo la kutunza mazingira na kuongeza pato.



Popo wa Pemba anavyonekana akiwa na tunda mdomoni

# PROGRAMU YA MASOKO, UONGEZAJI THAMANI NA HUDUMA ZA KIFEDHA VIJIJINI

Na Sabiha Kessi

Programu ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini (MIVARF) ni mpango wa miaka saba ambao utekelezaji wake umeanza rasmi mwezi wa saba mwaka 2011. Programu hii inagharamiwa na Serikali ya Tanzania ikishirikiana na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Taasisi ya Mapinduzi ya Kijani Africa (AGRA). Aidha, Programu hii itatekelezwa Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Programu hii inalenga kuchangia na kufanikisha malengo ya Mpango Mkakati wa Sekta ya Kilimo na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA) utekelezaji wa mikakati hii unatarajiwa kuongeza kipato, uhakika wa chakula, uzalishaji na tija.

Lengo kuu la Programu hii ni kufanikisha azma ya Serikali ya kupunguza umaskini na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi endelevu kwa kuziwezesha kaya za vijijini kujiongezea kipato na usalama wa chakula. Programu itafanikisha malengo yake kwa kuboresha miundo mbinu ya masoko, kuongeza thamani mazao ya kilimo, kupanua wigo wa huduma za kifedha zipatikanazo vijijini na kuwajengea wananchi waishio vijijini uwezo wa kuyafikia masoko.

Walengwa wa Programu hii watatoka katika mikoa yote ya Zanzibar. Aidha, walengwa watalazimika kufata vigezo vilivyowekwa ili kushiriki katika Programu. Uimarishaji wa miundombinu ya masoko, uongezaji wa thamani ya mazao mbali mbali utazingatiwa, ambapo walengwa wa Programu hii ni pamoja na wakulima wadogo wadogo, wavuvi, wafanya kazi za mikono, wajasiriamali pamoja na wafanyabiashara vijijini. Walengwa wangine ni asasi ndogo ndogo za kifedha zinazotoa huduma vijijini, vikundi vya ushirika usindikaji wa mazao na utafutaji wa masoko vijijini na ushiriki wa wanawake katika vikundi utapewa kipaumbele.




Makamu wa Pili wa Raisi Mhe. Balozi Seif Ali Iddi akiwa pamoja na Mhe Ramadhan A. Shaaban Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili kulia kwake na ndugu Affan O. Maalim, Katbu Mkuu wa Wizara hiyo wakiwa katika mkutano wa uzinduzi wa Programu ya MIVARF tarehe 29/11/2011 katika Ukumbi wa mkutano wa Salama, Bwawani.

**Programu hii imegawika katika vipengele vitatu:**

- Uendelezaji wa Miundo Mbinu na Mifumo ya Masoko,
- Uendelezaji wa Huduma za kifedha vijijini,
- Uratibu wa Programu.

Uendelezaji wa miundombinu na mifumo ya masoko utahusisha ujenzi na ukarabati wa barabara na maghala. Aidha, programu itaimarisha majengo ya masoko na miundombinu inayoyazunguka. Programu pia itajenga uwezo wa watendaji wa Serikali ili waweze kupanga, kutekeleza na kusimamia miundombinu ya masoko iliyoimarishwa, kusimamia mikataba mbali mbali na kamati za kusimamia miundombinu ya masoko ili kuwa na usimamizi endelevu wa miundombinu hiyo.

**Uongezaji Thamani Mazao**

Programu itatilia mkazo wa kuvijengea uwezo vituo vya kutoa mafunzo ya uhifadhi na usindikaji wa mazao.

Pia itakarabati na kununua vifaa kwa ajili ya vituo hivyo pamoja na kueneza teknolojia ya utunzaji wa mazao baada ya kuvunwa. Aidha, vikundi vitajengewa uwezo wa kuandika miradi itakayokubalika na mabenki. Pia itawaunganisha watoa huduma za kifedha na vikundi vya ushirika katika kuongeza thamani ya mazao yao. Wakulima watajengewa uwezo wa kupata masoko ya uhakika ya mazao yao, kupata taarifa za masoko kwa kushirikiana na watu na makampuni binafsi (PPP). Kazi za programu katika sehemu hii ni pamoja na:

i. Kuwajengea uwezo walengwa katika maswala ya masoko na uongezaji thamani na kutoa mafunzo kwa wawezeshaji;

ii. Kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wakulima, wasindikaji na wafanyabiashara katika kunadi mazao na;

iii. Kujenga uwezo wa walengwa katika mfumo wa upashanaji taarifa za masoko kwa kuzingatia misingi ya ushirikiano wa sekta binafsi na Serikali.

Uendelezaji wa Huduma za kifedha vijijini Kipengele hiki kitatekelezwa katika maeneo mawili muhimu nayo ni:

Uendelezaji wa Huduma za Kifedha kwa Kupitia Asasi Ndogo Ndogo za Kifedha - zitajengewa uwezo wa kifedha vijijini zikiwemo asasi zisizo rasmi kama upatu na SACCOS na Benki za Wananchi ili ziweze kuongeza wigo wa huduma zake vijijini. Kazi za msingi zitakazotekelezwa na programu hii katika eneo hili ni pamoja na:

i. Kuzijengea uwezo na kuziwezesha asasi ndogo ndogo za kifedha zisizo rasmi kuwa mfumo wa habari za masoko ili ziwe endelevu kwa kuzipa fursa ya kukua na kuingia katika kundi la asasi rasmi za kifedha na pia kuziunganisha na taasisi za fedha. Aidha, msukumo utawekwa katika kuzihamasisha asasi hizi kuunda mitandao itakayoziwezesha kuweka nguvu ya pamoja kupata na kutoa huduma za kitalaamu.

ii. Kuvijengea uwezo vyama vya akiba na mikopo (SACCOS) ili viwe endelevu.

iii. Kushirikiana na asasi za kifedha kwa lengo la kufikisha huduma vijijini mkazo utakuwa katika kuwafikia wanawake vijijini.

**Uratibu wa Programu**

Programu itaratibiwa na Ofisi Kuu ya Uratibu iliopo Arusha, kwa upande wa Zanzibar programu hii inaratibiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili ambapo ofisi yake itakuwa ndani ya jengo la Wizara Darajani. Lengo la uratibu ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa MIVARF unakuwa endelevu kama ulivyokusudiwa hata baada ya Programu kumaliza muda wake. Programu itafanya yafuatayo:

**Kujenga Uwezo wa Wakulima Katika Masuala ya Masoko**

i. Kuratibu kazi za wadau watakaotekeleza Programu,

ii. Kusimamia masuala ya kifedha ya programu;

iii. Kupanga, kufuatilia na kutathmini utendaji wa Programu na matokeo yake na kuzingatia masuala ya jinsia,

iv. Kutoa ushauri wa kitalaamu kwa watekelezaji wa Programu.

**Matokeo ya Programu**

Miundombinu ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini inatarajiwa kuzifikia moja kwa moja kaya zilizopo vijijini.

**Uendelezaji wa Miundombinu ya Masoko**

Mkazo utakuwa ni kuimarisha fursa za masoko na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo ambayo yataongeza kipato cha kaya

i. Kuimarika kwa miundombinu na mifumo ya masoko;

ii. Kushuka kwa gharama za uendeshaji;

iii. Kuongezeka uzalishaji;

iv. Kuwa na uhakika wa chakula;

v. Kupungua kwa upoteaji wa mazao baada ya kuvunwa; na

vi. Kuongezeka kwa ubora na thamani ya mazao ya mkulima, ajira isiyotokana na kilimo na kipato.

Mafanikio mengine yanayotarajiwa kupatikana kutokana na utekelezaji wa MIVARF ni pamoja na kuwepo kwa vikundi vya wazalishaji na masoko ambayo ni endelevu na kuwepo wadau wa sekta binafsi watakaojiingiza katika kazi za kilimo.

# Matukio ka



Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Machano Othman Said wa kwanza kulia, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo akiwa kushoto na Mwakilishi Mkaazi wa Tanzania wa Shirika la Chakula Duniani (WFP) Bwana Richard Ragan wakiwa katika makabidhiano ya kompyuta kwa ajili ya kuimarisha kitengo cha utoaji wa taarifa za tahadhari ya mapema cha Idara ya Uhakika wa Chakula na lishe.



Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzib
Programu ya Masoko, Uongezaji thamani
uzinduzi wa Programu hiyo tarehe 30/11/201
Hoteli ya Bwawani, Zanzibar.



Bwana Khamis Uledi Sheha wa Shehia ya Pujini,Chake Chake - Pemba aliyesimama akiwaelezea wanashehia umuhimu wa kuanzishwa kwa Kamati za shehia za Uhakika wa Chakula na Lishe wakati wa uteuzi wa wanajamii 30 uliofanyika katika shehia hiiyo ambao wataisaidia kamati hiyo katika kuibua mradi na utekelezaji wake. tarehe 8/12/2011



Wahitimu wa cheti cha kilimo, mkupuo wa ti
kupokea vyeti vyao iliyofanyika tarehe 30/12/20

# atika Picha



ar wakisikiliza kwa makini maelezo kuhusu na Huduma za Kifedha vijijini wakati wa 1 katika ukumbi wa mkutano wa Salama,



Mhe. Mwanajuma Majid, Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake akifunguwa mafunzo ya utayarishaji wa mpango kazi wa kamati za Uhakika wa Chakula na Lishe za shehia ya Pujini na Mbuzini, tarehe 4/12/2011 katika Ukumbi wa mkutano wa Uwanja wa Gombani, Pemba, kulia kwake ni Ndugu. Mzee Rajab mtaalamu wa Lishe wa Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe na kushoto kwake ni Ndugu Ali Haji, Mratibu wa FAO- Zanzibar.



sa na wa kumi wakiwa katika mahafali ya 011 katika chuo cha Kilimo, Kizimbani.



Ndugu Mberek Rashid Mkurugenzi wa Idara ya Kilimo akitoa maelezo kuhusu mipango ya maendeleo ya kilimo kwa Mgeni rasmi mama Asha Seif wakati wa maonyesho ya wajasiriamali yaliyofanyika Tunguu, Wilaya ya Kusini Unguja

# MAHAFALI YA 10 YA CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI

Na Sabiha Kessi

Chuo cha Kilimo Kizimbani kilicho chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili hivi karibuni kiliadhimisha mahafali ya kumi kwa wanafunzi waliomaliza mafunzo yao ya Astashahada ya Kilimo na Mifugo yanayotolewa kwa muda wa miaka miwili.

Jumla ya wanafunzi 132 wamemaliza mafunzo yao na kutunukiwa vyeti. Mahafali hayo yalihudhuriwa na viongozi mbali mbali wakiwemo Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili, Naibu Waziri wa Afya, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mgeni Rasmi katika mahafali hayo alikuwa Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili Mheshimiwa Ramadhan Abdalla Shaaban ambae alianza kwa kusema kuwa mwaka wa fedha ujao Serikali itaendelea na juhudi zake za kukisaidia Chuo cha Kilimo Kizimbani ili kuweza kuimarisha miundombinu pamoja na vifaa vya kufundishia.

Mhe. Shaaban aliyasema hayo wakati alipokua akiwatunuku vyeti wahitimu waliomaliza mafunzo yao ya kilimo na mifugo katika mahafali yaliyofanyika Chuoni hapo Kizimbani nje kidogo ya mji wa Zanzibar.

Amesema kuwa tokea Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Januari 1964, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekua ikitoa fursa kubwa kwa wakulima kujiendeleza. Katika msimu huu Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili imeongeza fursa hizo kwa wakulima wadogo wadogo kupitia vikundi vya ushirika kwa kuwapatia huduma bora za kilimo, zana za kisasa, kama matrekta, mbegu bora, mbolea na dawa za kuulia wadudu waharibifu na magugu kwa bei nafuu.



Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo ya Chuo cha Kilimo, Kizimbani Ndugu. Makame Salum, akipeana mkono na mhitimu baada ya kukabidhiwa cheti chake na mgeni rasmi Mhe. Ramadhani A. Shaaban.

Mhe. Shaaban amesisitiza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha mpango maalum wa mageuzi ya kilimo ambao umeelekeza kutoa huduma za kilimo na ushauri kwa wakulima ili waweze kuongeza uzalishaji kwa kiwango cha biashara badala ya kujikimu.

Aidha, amewataka wahitimu hao kuyatumia vizuri mafunzo waliyoyapata kwa kuweza kujiajiri wao wenyewe binafsi badala ya kusubiri ajira kutoka Serikalini.

Nae Mkurugenzi wa Chuo cha Kilimo Kizimbani Ndugu Mohammed Khamis Rashid amesema kuwa Chuo hicho kimeweza kupiga hatua mbalimbali zikiwemo upatikanaji wa nyenzo za kutendea kazi pamoja na kupata usajili katika baraza la vyuo Tanzania.

Mkurugenzi huyo, amefahamisha kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana chuo hicho kinakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo upungufu wa vifaa vya kusomeshea, miundombinu pamoja na maabara mambo ambayo hurudisha nyuma jitihada za walimu wakati wa kufundishia.

Utoaji wa vyeti kwa wahitimu ulifuatiwa na zawadi kwa wanafunzi bora na wafanyakazi waliomaliza muda wao wa utumishi chuoni. Wanafunzi bora waliotunukiwa zawadi ni Thabit Ali na Ramlat Ali Haji.

Akiendelea na nasaha zake kwa wahitimu na waliohudhuria, Mhe. Shaaban amefahamisha kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CCM inaendelea kutekeleza ilani ya uchaguzi ya mwaka 2010-2015 ambapo moja kati ya maelekezo muhimu yaliyomo ndani ya ilani hiyo ni kukiimarisha Chuo ili kiweze kutoa mchango mkubwa katika kuendeleza sekta ya kilimo hapa nchini kwani Chuo hicho hutoa wataalamu ambao huwa mstari wa mbele katika kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima na wafugaji.

# MCHANGO WA TASAF KATIKA USARIFU WA MAZAO, MANGAPWANI

Na Shabaan Abdulmalik

Mradi wa kusarifu matunda na kusindika katika mikebe Shehia ya Mangapwani ni mradi wa kundi maalumu la vijana wasio na ajira ambao umeanzishwa mwaka 2002 na kikundi cha kina mama kinachocheza upatu.

Mradi huu una wanachama wanane wote wakiwa wanawake. Kina mama hawa walianza kutengeneza achari ya embe mbichi na mbirimbi kwa njia za kienyeji bila mafanikio kwa kuwa achari hizo zilikuwa hazina ubora na ziliishia kuharibika



Viongozi wa Kikundi usarifu wa mazao cha Mangapwani: wakiwa na bidhaa walizozisarifu kutokana na matunda.

Baada ya kupata mafunzo kutoka kwa mtaalamu wa usarifu wa matunda wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, hivi sasa wamepata taaluma ya kutosha juu ya kusarifu na kuhifadhi matunda ya aina mbalimbali yakiwemo mananasi, machungwa, embe, ndimu, mbirimbi, tungule na ndizi na inategemea upatikanaji wa matunda katika misimu.

Kikundi hicho kwa hivi sasa kinaendelea na kazi za usarifu wa matunda, kuyasindika na kuyauza. Miongoni mwa matunda yanayosarifiwa ni pamoja na Tungule, Nanasi na Chungwa kwa kuyatengeneza Jamu, Ndimu na Embe hutengeneza achari.

Vilevile Tungule hutengenezewa chatne, wanatengeneza sosi inayotokana na pilipili na achari ya mbirimbi ya kuanika na kupika mapishi yote haya yanachanganywa na viungo maalumu ambavyo ni virutubisho mwilini na vina ladha nzuri. Kina mama hawa kwa kawaida hawatumii kemikali yoyote katika kusarifu matunda yao.

Kikundi hiki cha Mangapwani kimepatiwa jumla ya shilingi milioni 11.9 kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF. Aidha, mchango wa nguvu za wanakikundi hiki umepelekea kuongeza nguvu na sasa wameweza kujenga Ofisi yao, kununua vifaa vya mapishi na wamepata mafunzo, maalumu ambapo hayo yote yameweza kuwaletea mafanikio katika utekelezaji wa kazi zao za kila siku.

Mafanikio mengine waliyoyapata wanakikundi hawa kupitia TASAF ni pamoja na kujitangaza katika maonesho mbalimbali yakiwemo ya nane nane pia wameweza kujifunza mbinu mpya za kazi zao na kuongeza kiwango cha ushindani kilichopo katika biashara yao kwa kulingana na mahitaji ya soko.

Kazi hii ya usarifu wa mazao imewapatia ajira viongozi na wananchi, hasa baada ya kupata vifaa ambavyo kwa sasa vinawawezesha kufanya kazi ya kutosha ya kulitafuta soko na kuandaa bidhaa kwa ajili ya soko hilo. Hata hivyo, kikundi bado kinaendelea kutafuta taaluma zaidi ya kusarifu na kuhifadhi matunda ili yaweze kutumika kwa muda mrefu na yawe na ubora.

# USARIFU WA MAZAO YA KILIMO

Na Mussa H. Makame

Kwa muda mrefu wakulima wa visiwa vya Unguja na Pemba wamekuwa na kilio cha kukosa soko la uhakika kwa mazao yao. Hii ni kwa sababu mazao hayo ni ya msimu na pia yanakomaa katika kipindi kimoja; pia wakulima wengi wanakosa taaluma na nyenzo za kuyahifadhia mazao yao kwa matumizi ya baadae.

Taarifa za utafiti zinaonesha kuwa takriban asilimia 40 ya muhogo unaolimwa hapa Zanzibar unaharibika au unapotea baada ya kuvunwa. Hali hii pia inawezekana kuwepo kwa mazao mengine ambayo hayajafanyiwa utafiti.

Hali hii husababisha hasara kwa wakulima pamoja na kukata tamaa kwa vile wanahisi kuwa wamepoteza nguvu zao bila ya mafanikio. Tatizo hili kwa kiasi kikubwa linatokana na kuanguka kwa bei ya mazao hayo hasa wakati wa msimu wa mazao husika mfano zao la Embe , Machungwa na mazao mengineyo.



Jengo la usarifu wa mazao linaloendelea kujengwa katika kituo cha Kilimo Kizimbani kwa ajili ya kuwasaida wakulima pamoja na wajasiriamali kupata mafunzo ya usarifu wa mazao ya kilimo.

Mpango wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini umezingatia uwepo wa tatizo hili kwa kusema kuwa mfumo mbaya wa soko la bidhaa za kilimo na upotevu wa kuharibika kwa mazao baada ya kuvunwa ni miongoni mwa mambo yanayokwamisha maendeleo ya Sekta ya Kilimo hapa Zanzibar. Vile vile Sera ya Kilimo ya Mwaka 2002 inatilia mkazo suala la uekezaji katika usarifu wa mazao na kuongeza thamani mazao ya Kilimo ili kuwa na ukuaji endelevu wa kiuchumi na kupunguza umasikini.



Baadhi ya bidhaa zilizosarifiwa na wakulima wa Zanzibar kutokana na mafunzo ya usarifu wa mazao ili kuyaongezea thamani.

Uekezaji katika usarifu wa mazao unaweza kuwa ni chanzo muhimu cha kiuchumi na ajira kwa vijana na wanawake pamoja na watu wengine ambao kwa njia moja ama nyengine wamekosa ajira katika sekta rasmi; hasa kwa vile kilimo pamoja na sekta nyengine hazijaweza kutoa ajira

za kutosha kwa wananchi wa Zanzibar. Hata hivyo watu wengi wana mtazamo mbaya dhidi ya bidhaa za kilimo zilizosarifiwa na wazalishaji wadogo wadogo hapa Zanzibar. Bidhaa hizo zinaonekana kuwa ni za kiwango duni ikilinganishwa na zile zinazotoka nje ya nchi au hata Tanzania Bara.

Kwa kuzingatia uzito wa tatizo hili, Wizara ya Kilimo na Maliasili ya Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Mashirikiano ya Kimataifa la Korea (KOICA), ipo katika matayarisho ya Mradi wa usarifu wa mazao ya kilimo hapa Visiwani Unguja na Pemba kwa njia ya kisasa.

Mradi huo una lengo la kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo baada ya kuvunwa, kuongeza chakula na lishe, kukifanya chakula kuwa salama kwa walaji, chakula kukaa kwa muda mrefu bila ya kuharibika sambamba na kupunguza umasikini wa kipato kwa wakulima.

Vile vile Mradi huo umelenga kuwajengea uwezo wakulima juu ya usarifu wa mazao ya kilimo na Ujasiriamali pamoja na kutoa huduma za udhibiti wa ubora kwa bidhaa zinazozalishwa kwa lengo la kuongeza ajira na kipato kwa wazalishaji.

Aidha, hatua inayoendelea hivi sasa ni ujenzi wa Kituo cha mafunzo ya usarifu wa mazao ya kilimo kwa wakulima pamoja na wajasiriamali katika visiwa vya Unguja na Pemba. Kituo hicho kipo katika eneo la Chuo cha Kilimo, Kizimbani Wilaya ya Magharibi Unguja ambapo kimewekwa Jiwe la msingi tarehe 7/01/2011 na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Idd. katika sherehe za kuadhimisha miaka 47 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya tarehe 12/01/1964.

Kwa sasa mradi wa Usarifu wa Mazao ya Kilimo unaendelea na utafiti juu ya hali ya usarifu wa mazao ya kilimo ilivyo hapa Zanzibar. Utafiti huu pamoja na mambo mengine utawatambua wajasiriamali wanaojishughulisha na usarifu wa mazao ya kilimo mahali walipo, bidhaa wanazozalisha, uwezo wao wa kuzalisha, vifaa na njia wanazotumia kusarifu mazao hayo.

Pia kuzijua tasisi zinazowaendeleza wajasiriamali hao, upatikanaji wa mafunzo na aina ya mafunzo pamoja na kujua hali ya usajili kwa wazalishaji hao sambamba na kufahamu matatizo yanayokwamisha ukuaji wa biashara zao baada ya kuzalisha ili kutafuta njia muafaka. Matokeo ya utafiti huo yatatoa mwanga juu ya namna ya kuwaendeleza wajasiriamali katika usarifu wa mazao. Matokeo haya yanatarajiwa kutolewa mara tu baada ya kukamilika kwa utafiti.

Bila shaka utekelezaji wa Mradi usarifu wa mazao ya kilimo utaleta faraja kubwa kwa Wakulima na Wajasiriamali wanaosarifu mazao ya kilimo, sambamba na kuwapunguzia ukali wa maisha wakazi wa mijini na vijijini kwa kupata fursa ya kujiajiri wenyewe. Hata hivyo wananchi wenyewe wanapaswa kuwa tayari kutumia fursa na huduma zitakazotolewa katika Kituo cha Usarifu wa Mazao ya Kilimo huko Kizimbani.



Ndizi zilizoharibika sokoni kutokana na kukosekana kwa miundombinu ya usarifu wa mazao.

# UMWAGILIAJI MAJI NDANI YA GREENHOUSE

Na Amour U. Vuai

Micro-irrigation huu ni mfumo wa umwagiliaji maji wa mazao unaofanyika ndani ya eneo maalumu lililojengwa kwa kutumia vifaa vya plastiki au vioo (green house). Mazao yanayozalishwa kupitia mfumo huu ni Maua, mboga mboga kama vile Tungule, Pilipili mboga, Matango na mazao mengine. Umwagiliaji huu ni wa kisasa na hufanyika zaidi katika nchi zilizoendelea, hata hivyo hivi sasa umeanza kueleweka na kutumika katika baadhi ya maeneo ya wakulima wa Zanzibar.

Awali ukulima huu ulikuwa ukifanyika kwenye maeneo ya utalii kwa upandaji wa maua Kiwengwa. Kwa vile visiwa vya Zanzibar vina uchache wa ardhi kama ilivyo kwenye visiwa vyengine duniani, kilimo hiki kinahitajika sana, kwani wakulima wanaweza kutumia eneo dogo kwa kuzalisha mazao mengi na bora.



Greenhouse inayotumiwa na ndugu Othman Omar Juma mkulima wa Masingini, Wilaya ya Magharibi Unguja katika kuimarisha kilimo cha mbogamboga cha umwagiliaji maji.

**Faida zinazopatikana kwa umwagiliaji maji ndani ya green house:**

- Kupata mavuno makubwa na yenye ubora;
- Maradhi na wadudu waharibifu ni rahisi kudhibitiwa;
- Matumizi madogo ya kemikali;
- Hauhitaji wafanyakazi wengi katika kuhudumia;
- Huleta ufanisi mkubwa katika utumiaji maji;
- Unaweza kuchanganya maji na mbolea;
- Hupunguza ukuwaji wa magugu na;
- Unatumia njia ya kilimo cha kisasa.

**Hasara za umwagiliaji maji ndani ya greenhouse.**

- Gharama za kuanzia ni kubwa;
- Unahitaji utaalamu ili kuendesha mfumo huu;
- Mkusanyiko wa chumvi kwenye sehemu zinazoroa maji hupelekea kufa kwa mimea.



Mitungule iliyopandwa ndani ya greenhouse ya mkulima wa mboga mboga wa Masingini.

**Aina za greenhouse**

1. Greenhouse za nyumbani (home greenhouse)
2. Greenhouse za kusimama (free stand structure)

**Greenhouse za nyumbani**

Aina hizi za greenhouse mara nyingi huwa maeneo ya nyumbani, pia zinaweza kushikana na ukuta wa nyumba kwa upande mmoja na upande mwengine kubakia paa (top sheet) kuelekea upande wa chini, ambalo ni maalumu kwa kupunguza mionzi ya jua na matone ya mvua.

Ukubwa wa greenhouse unategemea na upatikanaji wa vifaa kutoka katika kiwanda husika lakini kiwango cha kawaida ni mita

# MAFANIKIO YA UMWAGILIAJI MAJI WA BONDE LA KIANGA MWEMBE MSALA

Na Shaaban A. Malik

Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji maji Shehia ya Kianga – Mwembe msala ni mradi wa kusaidia wanajamii wenye uwezo wa kufanya kazi lakini hali zao za maisha ni za kipato cha chini. Mradi huu uliopo Shehia ya Kianga unawashirikisha wanajamii wapatao 100 wakiwemo wanawake asilimia 70. Uzinduzi wa mradi huu ulifanyika rasmi mwezi wa Agosti 2011 na kuanza utekelezaji mwezi huo huo 2011.

Bonde la Kilimo Kianga Mwembe Msala ni kwa ajili ya Kilimo cha Mpunga na Mbogamboga kwa kumwagilia maji kutoka katika chemchem za asili zilizopo eneo hilo, pamoja na kuwepo kwa vyanzo hivyo vya maji wananchi wa eneo hilo walikuwa wakilima kwa tabu, mara moja kwa mwaka kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza maji katika mashamba yao.

Hivi sasa Bonde la Kianga Mwembe Msala lina jumla ya mita 450 za Mtaro wa saruji na milango ya kudhibiti maji ambayo yanasafirishwa kutoka katika vianzio mpaka kwenye mashamba kwa muda mfupi. Wakulima wa eneo hili sasa wanalima Mpunga na mbogamboga mara tatu kwa mwaka ambapo wana uhakika wa kupata chakula chao. Pia maeneo yote yaliyozunguka bonde na vianzio vya maji yamepandwa miti na yanalindwa kwa uhifadhi wa mazingira. Wananchi wa eneo hilo kupitia programu ya TASAF wamepatiwa elimu ya kuhifadhi fedha, usimamizi wa miradi na maarifa ya kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji.



Wakulima wa bonde la Kianga Mwembe msala wakiwa katika ujenzi wa mtaro wa kumwagilia maji.

Kazi kubwa iliyofanywa na mradi huu ni kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo uhifadhi wa chemchem za maji na ujenzi wa mitaro ya saruji kwa ajili ya kumwagilia maji mashamba ya mpunga na mbogamboga yapatayo ekari 60.

TASAF imetoa mafunzo ya usimamizi wa fedha na miradi kwa walengwa wa mradi huu pamoja na kuwapatia fedha za matumizi baada ya kumaliza kiasi fulani cha kazi ili kujikimu kimaisha. Jumla ya shilingi milioni 16. 6 zilitumika kuwalipa walengwa hao ikiwa ni asilimia 50 ya gharama za mradi huo.

Mafanikio ya Mradi wa Umwagiliaji Kianga Mwembe Msala yametokana na msaada wa shilingi milioni 33.3 kutoka TASAF na wananchi walipata posho dogo la kusaidia maisha yao, kiasi chengine cha fedha wakaweza kununua vifaa na kutekeleza kazi walizojipangia kwa wakati. Mategemeo makubwa waliyokuwa nayo ya kujitegemea kwa chakula na fedha yaliwapa ari ya

# Jarida la KILIMO

Toleo la Nane
Oktoba - Disemba, 2011

utekelezaji wa mradi wao.

Mafanikio mengine ya mkulima mmoja mmoja yanasimuliwa na Mzee Mussa Malecha Mafula ni mzee wa makamo ambae ni mkulima wa matango katika eneo la Kianga mwembe msala, anasema katika eneo lake dogo anavuna vipolo 10 hadi 13 kwa siku na mavuno ni kila baada ya siku moja, bei ya kipolo cha matango wakati wa msimu mzuri shilingi 30,000, maana yake ni kuwa kila baada ya siku moja mzee huyu anafanya mauzo ya shilingi 300,000.

Aidha, wakulima wa eneo hili wameanza kuiga na kujifunza maarifa ya ukulima wa mbogamboga kutoka kwa mzee huyo pamoja na usimamizi wa Afisa wa elimu kwa wakulima wa eneo hilo, kwani hapo kabla eneo hilo lilikuwa likiachwa bila kulimwa baada ya mavuno ya mpunga, sasa wakulima wengi wamejifunza na kwa sababu ya miundombinu iliopo eneo kubwa linalimwa mbogamboga.

Mzee Malecha sasa ana uhakika wa chakula chake, akiba na mahitaji muhimu ya maisha yake pia ameweza kuajiri watu wengine katika shamba lake.



Wakulima wakifarijika kutokana na miundombinu bora ya umwagiliaji maji katika bonde la Kianga Muembe msala.

Hapana shaka kama utafika katika eneo la Kianga mwembe Msala utaona mabadiliko makubwa kutokana na kuwepo kwa mradi wa wananchi uliosaidiwa na TASAF, kuwepo kwa miundombinu ya kumwagilia kumesababisha maji kuenea katika mashamba kwa ufanisi. Aidha, wakulima wamejifunza matumizi ya mbegu bora na mbolea, mpango wa kilimo cha kisasa, usimamizi na matengenezo ya mfumo wa kumwagilia. Wakulima wa Mwembe msala pia wameanzisha Jumuiya ya watumiaji wa maji ambayo ina dhamana ya uendeshaji, matengenezo na usimamizi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili imeweka wataalamu wa kilimo cha kumwagilia kusaidia sehemu hiyo.

Uongozi wa bonde la Kianga mwembe msala umesema: ni muhimu kuhakikisha vyanzo vya maji vinalindwa na kuhifadhiwa kwa matumizi endelevu. Kwahiyo watajitahidi kuendelea kutafuta utaalamu wa uzalishaji pamoja na masoko kwa bidhaa zao.


P. O. Box 159 Zanzibar, Simu: +255 24 2230986, Fax: +255 24 2234650
Barua pepe: kilimo@zanlink.com, Tovuti: www.kilimoznz.or.tz